# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,

**BARAZA LA MADIWANI**

## TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 25/10/2023

### 1.0. UTANGULIZI

**Mhe. Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii itagusa Maeneo yafuatayo: -

1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA KWANZA
2. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ROBO YA KWANZA
   - 2.1 TAARIFA YA MIRADI YA RUZUKU SEKONDARI
   - 2.2 TAARIFA YA MIRADI YA MAPATO YA NDANI ROBO YA KWANZA
3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KATIKA ROBO YA KWANZA
4. HITIMISHO



CamScanner

## 1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA KWANZA

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Hadi kufikia 30 Septemba mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 3,419,053,762.97 sawa na asilimia 23 ya makisio ya bajeti ya Mapato ya ndani ya Mwaka 2023/2024.

## 2. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ROBO YA KWANZA

### 2.1 TAARIFA YA MIRADI YA RUZUKU

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika kipindi hiki, Halmashauri yetu ilipokea jumla ya shilingi **68,900,000/=** kutoka Serikali Kuu kupitia program ya EP4R kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 3 ya matundu 9 ya vyoo katika shule ya Sekondari Bwiru Wasichana.

### 2.2 MIRADI YA MAPATO YA NDANI ROBO YA KWANZA 2023/2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa robo ya kwanza, kiasi cha shilingi **1,505,686,804.81** ambazo ni fedha za mapato ya ndani, zilielekezwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ufuatao:

i. Shilingi 446,522,417.00 zimetumika kulipa fidia ya kwa Wananchi-Barabara Mhonze, Sangabuye na Rugeye
ii. Shilingi 227,103,021.84 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara-Kangaye Road -Maduka Tisa, Nyambiti
iii. Shilingi 191,000,000.00 kwa ajili ya kuchangia mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
iv. Shilingi 151,192,701.55 kwa ajili ya umaliziaji wa wodi katika Hospitali ya Wilaya
v. Shilingi 135,670,841.61 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya lami Hospitali ya Wilaya
vi. Shilingi 82,831,340.00 kwa ajili ya Mradi wa tofali
vii. Shilingi 74,930,000.00 kwa ajili ya kuwezesha taarifa za Miradi ya Kamati ya Bunge (LAAC) na tathimini (M&E)
viii. Shilingi 70,550,368.63 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Nyamhongolo ya Daladala
ix. Shilingi 41,493,166.00 kwa ajili ya ununuzi wa POS 50



CamScanner

x. Shilingi 40,790,324.78 kwa ajili ya ukarabati na samani kwenye nyumba ya Mkurugenzi.
xi. Shilingi 19,318,323.40 kwa ajili ya ujenzi wa choo Nyamuhongolo(Nanenane)
xii. Shilingi 14,584,300.00 kwa ajili ya kuwezesha maonesho ya nanenane kwa mwaka 2023
xiii. Shilingi 6,700,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya umeme na maji katika shule ya Msingi Busenga Kata ya Buswelu.
xiv. Shilingi 3,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa matundu 4 ya vyoo soko la Kitangiri

**Note:** Aidha katika kipindi hiki Halmashauri imeandaa zabuni ya ununuzi wa mitambo ya kutengeneza barabara na kutangaza katika mfumo wa manunuzi wa Nest.

Kwa kipindi hiki Halmashauri imefanikiwa kuomba maombi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Serikali Kuu yenye jumla ya shilingi bilioni 2.9 ambayo tunategemea kuipokea muda wowote kuanzia sasa. Fedha hiyo itatekeleza Miradi ya Afya na Elimu katika Kata zetu.

## 3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 14/07/2023, Mwenge wa Uhuru uliwasili Wilaya ya Ilemela ukitokea Wilaya ya Ukerewe. Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa katika Kata 6 kati ya 19 za Wilaya ya Ilemela kwa umbali wa km 57, ambapo jumla ya Miradi 4 na shughuli 7 zenye thamani ya shilingi **1,353,420,169.62** ilitembelewa. Mradi 1 uliwekewa Jiwe la msingi, Miradi 2 ilizinduliwa, Mradi 1 ulikaguliwa, shughuli 6 zilikaguliwa na shughuli 1 iliimarishwa.

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Mnamo Tarehe 17/07/2023 Mhe. CPA. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza alifika katika stendi ya Mabasi Nyamhongolo kwa lengo la kufanya ukaguzi na kuongea na wamiliki wa mabasi pamoja na wadau mbalimbali wa stendi. Pamoja na mambo mengine aliwataka wamiliki wa mabasi "TABOA" kuona namna ya



CS CamScanner

kuhakikisha mabasi yaendayo Mikoani yanatumia pia stand ya Nyamhongolo na kuwataka mamlaka za usimamizi/udhibiti LATRA na RTO kuwa sehemu ya kufanikisha hili na kusisitiza kuwa, *"Sisi tunatakiwa kuwa vinara katika kutengeneza mazingira mazuri ili sekta binafsi waweze kufanya vizuri"*.

Vilevile, tarehe 13/09/2023 Mhe. CPA. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza alikabidhiwa miundombinu ya Elimu Msingi kupitia Mradi wa BOOST iliyotekelezwa katika Manispaa ya Ilemela ambapo alizindua Shule mpya ya Msingi ya Butuja iliyopo Kata ya Kahama. Mkuu wa mkoa alisistiza kuwa, wazazi, walezi na wanafunzi wahakikishe kuwa utoro haukubaliki Mwanza, wanafunzi wote waende shule. Miradi ya BOOST iliyotekelezwa Manispaa ya Ilemela iligharimu kiasi cha shilingi 1,574,900,000.00 na yote imekamilika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 13/07/2023 matokeo ya kidato cha sita kwa mwaka 2023 yalitangazwa. Katika Manispaa yetu, kati ya wanafunzi 811 waliofanya mtihani katika shule 8 za serikali na binafsi, wanafunzi 265 walipata daraja la 1, wanafunzi 400 walipata daraja la 2, wanafunzi 143 walipata daraja la 3, wanafunzi 2 walipata daraja la 4, na mwanafunzi 1 alifeli.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mnamo tarehe 26 Mwezi Julai 2023 Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Hassan Masala alipokea msaada wa madawati 100 yenye thamani ya shilingi 9,000,000.00 kutoka Benki ya NMB (Mwanza). Vilevile, NMB Benki walimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ilemela vifaa tiba mbalimbali ikiwemo vitanda na mashuka vyenye thamani ya takriban shilingi 7,000,000.00. Vifaa hivyo tayari vimesambazwa katika shule na vituo vya afya vyenye uhitaji.



CamScanner

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 28 Mwezi Julai 2023 Mheshimiwa Angeline Sylvester Mabula Mbunge wa Jimbo la Ilemela alifanya Ziara katika jimbo lake. Katika ziara hiyo, alifanikiwa kuweka jiwe la msingi katika jengo la Ofisi ya Kata ya Mecco ambalo limefikia hatua ya boma ambapo tayari limegharimu takriban shilingi milioni 8.93. Pia, Tarehe 29 Julai 2023 na tarehe 16 Septemba 2023 Mheshimiwa Mabula alikabidhi jumla ya mitungi 900 ya nishati mbadala ya gesi kwa kinamama wajasiriamali katika kata 19 za Manispaa ya Ilemela. Zoezi hili ni kwa ajili ya kuunga mkono kampeni ya Kitaifa ya kutunza mazingira. Sambamba na hayo, Mheshimiwa Mabula amegawa vifaa vya TEHAMA aina ya kompyuta, Projekta, na Printa kwa shule za Sekondari 3 za Manispaa ya Ilemela ambazo ni Bwiru Wasichana, Sangabuye, na Angeline Mabula.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 11 mwezi Agosti 2023 Baraza la Madiwani la Mwaka lilifanya uchaguzi wa awamu ya 3 wa Naibu Meya wa Manispaa ya Ilemela ambapo Mheshimiwa Manusura Lusigaliye, Diwani wa Kata ya Buzuruga alichaguliwa katika nafasi hiyo. Aidha Mhe. Hussein Magela alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Mhe. Godlisten Kisanga kuwa Mwenyekiti ya Kamati ya Mipango Miji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 10 mwezi Septemba 2023 Halmashauri yetu ilitembelewa na Baraza la Madiwani kutoka Mjini Kati Zanzibar. Wageni hao walilenga kujifunza mbinu mbalimbali katika ukusanyaji wa mapato, na kutembelea stendi yetu ya Nyamhongolo ambapo vyote hivyo walifanikiwa kama walivyokusudia.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 10 Septemba 2023 Halmashauri yetu ilipokea jumla ya vitabu 30,364 vyenye thamani ya shilingi 118,149,702.00 kutoka Serikali Kuu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Vitabu hivyo tayari vimekwishwa kugawanywa katika Shule zetu za



CS CamScanner

sekondari ikiwa na lengo la kukamilisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja mashuleni.

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Mnamo tarehe 13 mwezi Septemba 2023 wanafunzi wa darasa la saba katika Halmashauri yetu walishiriki kufanya mitihani yao ya kuhitimu Elimu ya Msingi. Katika halmashauri yetu, jumla ya watahiniwa 11,618 wakiwemo wasichana 6,115 na wavulana 5503 katika shule 76 za Serikali na shule 47 za binafsi waliungana na wenzao kote nchini kufanya mtihani huo.

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Mnamo tarehe 23 mwezi Septemba 2023 Mtahiki Meya wa Manispaa ya Ilemela Mheshimiwa Renatus Mulunga pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Wakili Kibamba Kiomoni Kiburwa walisaini mkataba wa ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 12.8 zitakazogharimu kiasi cha shilingi 23.49. barabara hizo ni barabara ya Buswelu- Nyamadoke- Nyamhongolo yenye kilometa 9.5, na Barabara ya Buswelu- Busenga- Cocacola yenye kilometa 3.3.

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Mnamo Tarehe 25 mwezi Septemba 2023 Mkurugenzi wa Campus ya IFM Simiyu na Mratibu Msaidizi wa HEET Ndugu Ibrahim Kikwiye alifika katika Halmashauri yetu, Katika kikao chake pamoja na Baraza la Madiwani, Menejimenti pamoja na Wawakilishi kutoka Kata ya Kiseke alieleza Chuo cha IFM kitajengwa Manispaa ya Ilemela, Kata ya Kiseke kupitia Mradi wa (Higher Education for Economic Transformation) HEET ambao utatekelezwa kupitia fedha za mkopo kutoka benki ya Dunia ambapo takriban kiasi cha shilingi Bilioni 4.767 zitatumika.



CamScanner

## Hitimisho

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri yetu, pia tunapenda kumshukuru Mhe. Mbunge Angelina S. Mabula kwa kuendelea kuchochea na kuhamasisha utekelezaji wa Miradi katika Halmashauri yetu, pia tunamshukuru Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Waheshimiwa Madiwani, Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Wananchi wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Miradi ya Manispaa ya Ilemela.

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Naomba kuwasilisha.

Adv. Kibamba K. Kiburwa
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA
S.L.P. 735
MWANZA.
MANISPAA YA ILEMELA

CamScanner